

HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE



VIVUTIO VYA UTALII WILAYA YA SONGWE

1. Wanyamapori wanaopatikana ndani ya hifadhi ya Piti/Lukwati na Maeneo mengine ya mapori ya wazi ambao utalii mkubwa unaofanyika kwa sasa ni uwindaji, kutazama wanyama na kupiga picha kupitia kamapuni tatu za uwindaji wa kitalii za Old Nyika Safari, Safari Royal na Michel Mantheakis.



Tembo na Twiga hifadhi ya Piti/Lukwati



Nyati waliowindwa na wageni kitalu cha Chunya Msami ndani ya hifadhi ya Piti/Lukwati





Simba wanapatikana Maeneo mbalimbali ya Wilaya pamoja na ndege inayoleta watalii kuwinda hifadhi ya Piti/Lukwati



Sehemu ya kulia chakula wageni na mgeni aliyewinda mnyama aina ya palahala

2. Chemchem ya maji ya moto zinapatikana kata ya Gua na Ifwenkenya



Chechem ya maji moto kijiji cha Ileya kata ya Ifwenkenya

3. Mto Songwe wenye sifa ya Kubadili njia kila mwaka na una bionuwai nyingi



Mto songwe unavyoonekana kijiji cha Mbuyuni kata ya Mbuyuni

4. Ziwa Rukwa lenye mamba wengi kuliko maziwa yote Tanzania na linapatikana katika bonde la ufa. Katika Wilaya ya Songwe limezungukwa na kata sita za Manda, Mpona, Totowe, Mbangala, Uinde na Gua katika tarafa zote mbili



Boti ya Halmashauri ikiwa doria Ziwa Rukwa na muonekano wa Ziwa

5. Kanisa katoliki lilijengwa mwaka 1905 lililopo kata ya Galula



6. Makaa ya mawe yanapatikana kata ya Magamba na Namkukwe



Makaa ya mawe kata ya magamba

7. Mlima kwimba unaopatikana kata ya Kapalala ambao unatumika kwa ajili ya matambiko



Mlima kwimba kata ya Kapalala unavyooneka kutokea barabara kuu

8. Misitu ya miombo inapatikana maeneo yote ya Wilaya na inasifa ya kuchipua hivyo kusaidia miti ya asili kutotoweka. Lakini pia ni mizuri kwa ajili ya shughuli za uvunaji wa mazao ya misitu na ufugaji nyuki na makazi ya wanyamapori



Misitu ya miombo kata ya Ngwala na Kapalala

9. Hifadhi ya Wanayamapori ya kijiji cha Kapalala ambayo ina mbuga nyingi nzuri zinazovutia wanyamapori wa aina mbalimbali



Mkuu wa Wilaya na wakikagua uharibifu wa mazingira hifadhi ya wanyamapori ya kijiji cha kapalala

10. Msitu wa hifadhi wa patamela ambapo una safu ya milima na pia kuna madini ya dhahabu kwa sasa sehemu ya msitu huu kunafanyika uchimbaji mkubwa wa dhahabu na kampuni ya Shanta Gold mine



Sehemu ya msitu wa hifadhi wa Patamela